

HALMASHAURI YA MANISPAA YA MUSOMA


(Barua zote zipelekwe kwa Mkurugenzi wa Manispaa Musoma)

SIMU: 028-2622560/2622550

FAX: 028-2620550

E-mail: md@musomamc.go.tz

Tovuti: www.musomamc.go.tz



OFISI YA MKURUGENZI WA MANISPAA,
HALMASHAURI YA MANISPAA MUSOMA,
S.L.P. 194,
MUSOMA.

Tarehe: 10 Agosti, 2017

TAARIFA KWA UMMA

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Musoma Bi. Fidelica Godfrey Myovella anapenda kuutarifu umma Halmashauri ya Manispaa ya Musoma imevuka lengo la Makusanyo ya Ndani (Own Source) kwa mwaka wa fedha 2016/2017 kwa kukusanya asilimia 103.65

Makisio ya Makusanyo ya mapato ndani kwa mwaka 2016/2017 yalikuwa **Tsh.1,634,773,000.00** ambapo mpaka kufikia Juni 30.2017 Halmashauri ilikuwa imekusanya **Tsh. 1,694,508,366.32** sawa na asilimia 103.65

Vyanzo vya mapato vilivyofanya vizuri katika makusanyo ya ndani ni pamoja na Leseni ya Biashara, Leseni ya Vileo, Ushuru wa Machinjio, Ushuru wa samaki na Dagaa, Leseni za Mitumbwi, Ushuru wa Matangazo pamoja na ushuru wa Stendi za Magari.

Ufanisi wa Makusanyo haya umetokana na jitihada kubwa za watendaji wa Halmashauri katika kusimamia na kukusanya mapato pamoja na ushirikiano mkubwa uliopo miongoni mwa viongozi mbalimbali katika Halmashauri ya Musoma.

Mapato yaliyokusanywa kwa kiasi kikubwa yamesaidia uboreshaji wa huduma zitolewazo na Halmashauri ikiwa ni uboreshaji wa huduma za jamii kama Afya, Elimu pamoja na uwezeshaji wananchi kiuchumi.

Aidha, Mkurugenzi anapenda kuwashukuru wananchi wote pamoja na wafanyabiashara kwa kuendelea kulipa kodi na ushuru mbalimbali kwa maendeleo ya Manispaa yetu na kuwataka kuendelea na mwitikio huo katika mwaka wa fedha 2017/2018.

Mafuru Mjarifu

Afisa Habari/Uhusiano

Halmashauri ya Manispaa

Musoma.